



SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

WIZARA YA AFYA

**MWONGOZO WA KIWANGO CHA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA
KWA WAHUDUMU WA AFYA WA JAMII WA KUJITOLEA**

Kitengo cha Elimu ya Afya Zanzibar

Wakishirikiana na

Kitengo cha Mafunzo

Orodha ya Vifupisho

AIDs	Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)
ANC	Huduma za Kliniki kwa Mama Wajawazito
AYFSRH	Huduma Rafiki za Afya ya Uzazi kwa Vijana
CBHP	Mpango wa Afya ya Jamii
CHIS	Mfumo wa Taarifa za Afya ya Jamii
DHMT	Timu za Usimamizi wa Afya za Wilaya
CHVs	Wahudumu wa Afya wa jamii wa kujitolea
CHW	Wafanyakazi wa Afya wa Jamii
CSO	Asasi za Kiraia
DOT	Utumiaji wa Dawa Chini ya Uangalizi wa Moja kwa Moja wa Mhudumu wa Afya
DPs	Washirika wa Maendeleo
ECD	Makuzi ya Awali ya Mtoto
FBO	Mashirika ya Kidini
FP	Uzazi wa Mpango
GBV	Ukatili wa Kijinsia
HIV	Virusi Vya Ukimwi (VUU)
HPV	Virusi vya Papilloma
INGOs	Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Kiserikali
IPC	Mawasaniano ya Ana kwa Ana
IPs	Washirika wa Utekelezaji
IYCF	Lishe kwa Watoto Wachanga na Watoto Wadogo
LLITN	Vyandarua Vyenyeye Dawa ya Muda Mrefu
LMIC	Nchi Zenye Uchumi wa Chini na wa Kati/Wastani
M&E	Ufuatiliaji na Tathmini
MIP	Mwongozo wa Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya
MNCH	Afya ya Mama, Watoto Wachanga na Watoto Chini ya Miaka Mitano (5)
MOHSWEG C	Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto
MPDSR	Ufuatiliaji na Kukabiliana na Vifo vya Mama na Mtoto Wachanga
MUAC	Kipimo cha Uchunguzi wa Utapiamlo Kupitia Sehemu ya Juu ya Mkono Karibia na Bega
NCD	Maradhi Yasiyo ya Kuambukiza
NGO	Asasi Zisizo za Kiserikali
NTD	Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele
PAC	Huduma Baada ya Mimba Kuharibika
PHC	Huduma za Afya za Msingi
PMTCT	Kuzuia Maambukizi Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto
PNC	Huduma Baada ya Kujifungua
PORALGSD	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ
PPFP	Uzazi wa Mpango Baada ya Kujifungua
RCH	Afya ya Uzazi na Mtoto
RGoZ	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ)
RMNCAH	Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto Chini ya Miaka Mitano (5) na Vijana
SAM	Utapiamlo Mkali
SBCC	Ubadilishaji wa Jumla wa Tabia za Jamii
SHCC	Kamati Kiongozi za Afya za Shehia
TB	Kifua Kikuu
UHC	Upatikanaji/Utoaji wa Huduma za Afya kwa Watu Wote
WASH	Maji, Usafi wa Mazingira na Mwili
WIT	Shirika Lisilo la Kiserikali la Willows International Tanzania

WHO	Shirika la Afya Duniani
WRA	Wanawake Walio Katika Umri wa Kuweza Kupata Ujauzito
ZCHS	Mkakati wa Afya ya Jamii wa Zanzibar

Yaliyomo

ORODHA YA VIFUPISHO	i
ORODHA YA MAJEDWALI	v
Utangulizi.....	vi
Shukurani	vii
Sura ya 1	1
Madhumuni, Mpangilio na Matumizi ya Mwongozo wa Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHV).....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Madhumuni ya utayarishaji wa Kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa watoa huduma za afya wa kujitolea wa jamii	2
1.3 Mpangilio na matumizi ya Kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa Wahudumu wa Kujitolea wa Afya ya Jamii (CHV)	2
1.3.1 Mpangilio wa mwongozo.....	2
1.3.2 Walengwa wa mwongozo huu	3
Sura ya 2.....	4
Maeneo ya Programu ya Kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa Watoa Huduma ya Afya wa Kujitolea wa Jamii	4
2.1 Utangulizi.....	4
2.2 Mikakati na Programu Itakayotekelezwa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs)....	4
2.2.1 Seti ya Mikakati na 1: Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana (RMNCAH)	5
2.2.2 Seti ya Mikakati na 2: Lishe	6
2.2.3 Seti ya Mikakati na 3: Kifua Kikuu/VVU na UKIMWI	6
2.2.4 Seti ya Mikakati na 4: Malaria.....	7
2.2.5 Seti ya Mikakati na 5: Afya ya Mazingira, Maji na Usafi	7
2.2.6 Seti ya Mikakati na 6: Maradhi Yasiyoambukiza.....	7
2.2.7 Seti ya Mikakati na 7: Magonjwa Yasiopewa Kipaumbele.....	8
2.2.8 Seti ya Mikakati na 8: Ufuatiliaji na Tathmini.....	8
2.2.9 Programu mtambuka	9
Katika eneo hili, mambo yafuatayo yatajumuishwa:	9
SURA YA TATU	10
KIWANGO CHA HUDUMA CHA WAHUDUMU WA AFYA WA KUJITOLEA.....	10
3.1 Utangulizi.....	10
3.2 Huduma kwa kila mkakati	10
3.2.1 Seti ya Mikakati na 1: Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto Chini ya Miaka 5 na Vijana10 Programu mbalimbali za kiwango cha huduma kwa ajili ya Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto Chini ya Miaka 5 na Vijana zinaelezwa katika jedwali la 8 lifuatalo:.....	10
3.2.2 Seti ya Mikakati 2: Lishe	13
3.2.3 Seti ya Mikakati 3: Kifua Kikuu (TB), VVU na UKIMWI.....	14
3.2.4 Seti ya Mikakati na 4: Malaria.....	14
3.2.5 Seti ya Mikakati na 5: Afya ya Mazingira, Maji na Usafi	15
3.2.6 Seti ya Mikakati 6: Maradhi yasiyo ya kuambukiza.....	15
3.2.7 Seti ya Mikakati na 7: Magonjwa yasiyopewa kipaumbele	16
3.2.8 Seti ya Mikakati na 8: Ufuatiliaji na Tathmini (M&E)	16
3.2.9 Programu mtambuka	17
3.2.5.....	18
Marejeleo.....	19
Kiambatisho 1	21
Hadidu rejea kwa timu ya wataalamu wa afya ya jamii.....	21

Orodha Ya Majedwali

Jedwali 1: Mambo yaliyomo katika Mpango wa Mabadiliko wa Afya ya Uzazi, Afya ya Mama, Mtoto na Kijana	5
Jedwali 2: Orodha ya hatua na mambo yaliyomo katika seti ya upatikanaji wa lishe	6
Jedwali 3: Orodha ya Mikakati inayofaa kuchukuliwa katika programu za Kifua Kikuu/VVU NA UKIMWI	6
Jedwali 4: Orodha ya mikakati ya programu ya Malaria	7
Jedwali 5: Orodha ya hatua mbalimbali chini wa mpango wa Afya ya Mazingira, Maji na Usafi.....	7
Jedwali 6: Mikakati inayofaa kuchukuliwa dhidi ya Maradhi Yasiyoambukiza	7
Jedwali 7: Hatua za Maradhi yasiyopewa kipaumbele	8
Jedwali 8: Mikakati ya Utoaji wa Huduma kwa Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana	10
Jedwali 9: Orodha ya hatua, mikakati na huduma zilizomo katika kipengele cha lishe	13
Jedwali 10: Orodha ya Mikakati inayofaa kuchukuliwa katika programu za Kifua Kikuu/VVU NA UKIMWI	14
Jedwali 11: Mikakati ya kijamii kwa ajili ya Programu za malaria	14
Jedwali 12: Mikakati ya kijamii kwa ajili ya Afya ya Mazingira, Maji na Usafi.....	15
Jedwali 13: Hatua za afya ya jamii kuhusu Maradhi yasiyo ya Kuambukiza.....	15
Jedwali 14: Seti ya huduma za kijamii kwa ajili ya maradhi yasiopewa kipaumbele.....	16
Jedwali 15: Mikakati wa kijamii kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini	17
Jedwali 16: Kifurushi cha huduma ya jamii kwa ajili shughuli mtambuka.....	17


Mnamo mwaka 2011, Zanzibar iliunda mkakati wake wa kwanza wa Afya ya Jamii uitwao Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) kwa lengo kuu la kuimarisha miundo iliyopo na kuandaa mfumo wa pamoja wa uratibu wa hatua mbalimbali za kiafya katika Jamii. Wakati wa utekelezaji wa Mpango huo, fursa mpya ziliibuka. Lengo kuu la wakati huo lilikua ni kuimarisha ushiriki wa jamii katika usimamizi na uendeshaji wa mfumo wa afya, hasa huduma ya msingi ya afya kwa kuanzisha na kusaidia kazi za mifumo ya Afya iliyomo katika Shehia. Kisha, kuonesha mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na matumizi ya Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea (CHVs), Pia kuongeza uhitaji wa huduma za afya kama vile utoaji wa huduma za afya kwa wajawazito na huduma baada ya kujifungua. Kwa muda sasa, Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea (CHVs) wamethibitisha kuwa na mchango mkubwa katika kufikia matokeo mazuri ya kiafya hasa katika eneo la Afya ya Mama na Mtoto na kwa jamii ya Wazanzibari kwa ujumla.

Hata hivyo, mfumo huo haukusimamiwa vizuri na kada hiyo haikutambuliwa rasmi na kuwekwa katika mfumo rasmi wa afya na Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS). Kutokana na mahitaji ya kushughulikia changamoto na upungufu ulioelezwa hapo juu, na katika jitihada za kuinua na kudumisha huduma bora za msingi za afya, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa dhati kabisa waliona kuna umuhimu wa kushughulikia kasoro zilizopo za kiprogramu na kimuundo. Ili kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Afya katika Jamii, kulikuwa na haja ya kurekebisha mfumo wa afya kwa kuimarisha utekelezaji wa Huduma ya Afya ya Msingi (PHC), hili lilitekelezwa kwa lengo la kubadili mfumo wa utoaji huduma ambao ulikuwa wa ngazi ya juu tu na usio jumuishi na kupeleka mfumo wa afya katika ngazi ya jamii. Hivyo, Wizara hizi ziliamua kupitia na kuufanyia marekebisho Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) na kubainisha hatua zinazofaa za utekelezaji kupitia Programu au Mpango wa Afya katika Jamii (CBHP) uliopitiwa upya, ulifanywa kuwa jumuishi na kuboreshwa kulingana na mahitaji ya utoaji wa Huduma ya Msingi ya Afya (PHC).

Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) (2019-2025) upo tayari, umezinduliwa na unatumika. Mkakati huo unakwenda sambamba na mabadiliko, uvumbuzi na maendeleo mengine ambayo yanazingatia kuimarisha Huduma ya Msingi ya Afya. Vilevile kuimarisha huduma za jamii zinazotekelezwa na Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea (CHVs). Lakini, mkakati huo hautakuwa na faida ikiwa watekelezaji wakuu wanaounga mkono Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) hawatawapa Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea (CHVs) zana na miongozo maalumu ya kufanyia kazi ili kusimamia utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na utoaji huduma na usimamizi wa Mpango wa Afya ya Jamii.

Kutengenezwa kwa **Mwongozo** huu wa **Taifa kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs)** ni mfano hai wa namna Serikali, kwa kushirikiana na washirika wake wa maendeleo wanafanya kazi kwa pamoja ya kuutekeleza kwa vitendo Mpango Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS). Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefurahishwa na namna wadau mbalimbali pamoja na jamii walivyoshiriki kikamilifu katika mchakato wote wakati wa utengenezaji wa Mwongozo huu. Mwongozo huu unatoa muhtasari wa jumla unaohusu utoaji wa huduma za Afya ya Jamii kwa mapana yake kama inavyohitajika chini ya mamlaka ya Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. Mwongozo huu pia, unakusudiwa kutumika kama kielelezo cha taifa kuhusu masuala ambayo yatajenga ufahamu na ushiriki wa jamii kupitia Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. Vile vile, Wizara hizi mbili zimefurahishwa kuona kwamba Mpango Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar hapa Zanzibar unazidi kufanyiwa maboresho muhimu na kutolewa maelekezo ya namna nzuri ya utekelezaji wake. Ni mafanikio makubwa kufikia hatua hii ambapo Mpango Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) (2019-2025) sasa umetekelezwa kwa vitendo kupitia zana na miongozo mbalimbali ya CBHP iliyotengenezwa wakati wa mchakato huu na inayotarajiwa kuwaongoza wadau wote wanaotekeleza na wanaounga mkono Mpango wa Afya ya Jamii nchini.

Aidha, Wizara zote mbili zinawahimiza wadau wote wa afya na washirika wa maendeleo kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea wanatekeleza majukumu na kazi zao kwa mafanikio wakiongozwa na miongozo hiina zana hizi muhimu. Hakuna shaka kwamba, ushiriki wa jamii katika usimamizi wa mifumo ya afya hauepukiki na unafaida kubwa kwa jamii, na kwamba, utekelezaji wa viwango vilivyowekwa vya utoaji wa huduma za afya utaimarisha uhamasishaji wa shughuli za afya, udhibiti wa maradhi na kuimarisha matokeo bora ya afya kwa jamii ya Zanzibari.



.....
Dkt Fatma H. Mrisho
Katibu Mkuu
Wizara ya Afya

Shukurani

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, inapenda kutoa shukurani za dhati kwa mashirika na watu wote walioshiriki katika kusaidia utayarishaji wa miongozo na vitendea kazi mbalimbali vya Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) Zanzibar ambapo miongoni mwao ni Mwongozo huu wa Mafunzo wa Taifa kwa Kamati Kiongozi za Afya za Shehia (SHCCs). Watu binafsi na mashirika mbalimbali yamejitolea muda, juhudi na rasilimali zao kuhakikisha miongozo yote hii muhimu ya Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) inafanikiwa. Ili kuwepo kwa mpango madhubuti wa Afya ya Jamii, taasisi nyingi zililusika kwa namna tofauti kutokana na kwamba mchakato huu ulihitaji nguvu za pamoja za wadau wote nchini.

Pia, Serikali inapenda kuwashukuru wale wote waliotoa michango yao kwa njia mbalimbali wakiwemo wale waliofanya uchambuzi na upembuzi yakinifu, tathmini ya mahitaji yaliyopo, mapitio na maboresho katika hatua za mwisho, pamoja na uidhinishaji wa rasimu za miongozo na zana mbalimbali. Miongoni mwao ni Bwana Abdurahman Kwaza, kutoka Kitengo cha Elimu ya Afya (HPU) cha Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ambaye alitoa miongozo bora na usimamizi mzuri kwa kuratibu mchakato huo kwa niaba ya Wizara hizo.

Kwa uzito mkubwa, Serikali inapongeza sana mchango muhimu wa kiuongozi, ushauri, ufuatiliaji na uratibu wa karibu kutoka kwa Dk Salim Slim (Naibu Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya) ambaye amewezesha katika kufikia hatua hii. Wengine ni Bi Halima Khamis, Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Afya, Wizara ya Afya ambaye alikuwa karibu kila wakati kusaidia na kuongoza timu ya Kitengo cha Uhamasishaji wa Afya ya Jamii na timu ya washauri kila wakati ilipohitajika, Bwana Khalid Abdalla, aliyekuwa Kaimu Katibu Mkuu wa wakati huo wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ na Mwenyekiti wa Kamati ya Uendeshaji ya Mkakati wa Afya ya Jamii, timu ya wataalamu wa Huduma za Afya ya Jamii ya Zanzibar ambayo ilijumuisha wajumbe wake wote wanaohusika katika programu maalumu ya mpango wa afya pamoja na maafisa wawakilishi walioteuliwa kutoka katika Washirika wa Utekelezaji (IPs) na Washirika wa Maendeleo (DPs) ambao wanaunga mkono Mpango wa Afya kwa Jamii (CBHP). Vilevile, Serikali inapenda kuthamini mchango wa wafanyakazi wote wa kitengo cha Elimu ya Afya, IRCHP, HMIS, Malaria, Kifua Kikuu/UKIMWI, Chanjo (EPI), Lishe na Kitengo cha Mafunzo kwa kuwajibika bila ya kuchoka ili kuhakikisha miongozo hii inapatikana na ikiwa katika kiwango cha ubora mkubwa kwa ajili ya Programu ya Afya ya Jamii ikiwemo mwongozo huu wa Mafunzo wa Taifa kwa Kamati Kiongozi za Afya za Shehia (SHCCs).

Kazi hii isingefanikiwa bila jitihada na msaada wa kitaalamu na kifedha kutoka Shirika la Willows International. Juhudi zao na mchango wao umekuwa ni mkubwa mno. Wamechukua jitihada katika kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) (2019-2025) kwa vitendo kupitia utengenezaji wa miongozo na zana hizi na kufadhili shughuli na michakato yote iliyohusika kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa shukurani za dhati kwa Dr. Gokgol Turkiz (Rais na Mkurugenzi Mkuu, Willows International makao makuu), Dk. Muhadili Shemsanga (Mkurugenzi, WIT), Bwana Paul Mchau (Meneja wa Fedha na Utawala), Bwana Kahema Irema (Kiongozi wa Programu ya WIT Zanzibar), Dk. Mtumwa Kombo (Meneja wa Programu, Zanzibar), Bi Neema Sirima (Mratibu wa Programu), Mwanahamisi Kilongo (Afisa Tawala) na wafanyakazi wote wa WIT kwa ushirikiano mkubwa na msaada wao. Serikali pia inapenda kuwashukuru sana Global Fund kwa kuunga mkono jitihada za WIT kwa kuchangia msaada wa kitaalamu na kifedha ili kukamilisha miongozo na vitendea kazi hivi muhimu vya CBHP.

Mwisho kwa udhati, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua jitihada za kiufundi za timu ya Washauri Wataalamu ambao waliongoza mchakato na shughuli zote zilizosababisha kupatikana kwa miongozo na zana zote ikiwamo Mwongozo huu. Zaidi Serikali inapenda pia kumshukuru Bwana Selemani Mbuyita ambaye alikuwa Mshauri Kiongozi pamoja na wenzake Ndugu Issa Mussa, Dk. Yahya Ipuge na Dk. Emmanuel Matechi. Bidii yao na kujitolea kwao kutathaminiwa daima kwa kuweka alama katika Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) ya Zanzibar. Vivyo hivyo, shukurani na utambuzi maalumu unatolewa kwa Wasaidizi wa Utafiti ambao walishiriki katika kufanya uchambuzi na upembuzi yakinifu, tathmini ya mahitaji yaliyopo ambao uliweka msingi muhimu wa utengenezaji wa miongozo na zana za Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) wa kitaifa. Kwa wote waliotajwa na ambao hawajatajwa, Serikali inatambua kazi na mchango wao katika kukuza huduma za Afya ya jamii ambao utawezesha sana uimarishaji wa afya ya jamii kwa Wazanzibari.



.....
Dkt. Ali Said Nyanga
Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Na Elimu ya Afya
Wizara ya Afya

SURA YA 1

Madhumuni, Uundwaji na Matumizi ya Mwongozo wa Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs)

1.1 Utangulizi

Faida za Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHV) katika kudhibiti maradhi na kurekebisha tabia hatarishi zimejadiliwa sana katika nyaraka mbalimbali. Katika jamii zenye kipato cha chini na cha wastani (LMICs), Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHV) wameonekana kuwa na ufanisi katika kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na vile vya watoto, kabla na baada ya kujifungua, ambavyo kimsingi vinasababishwa na matatizo mbalimbali ya kiafya yanayoweza kuzuilika kirahisi. Kwa kuongezea, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea wamefanikiwa katika kuimarisha tabia bora za kiafya pamoja na unyonyeshaji maziwa ya mama, kufuata tiba ya VVU na ushauri nasaha, chanjo za utotoni, usafi wa mazingira, utunzaji wa mama kabla ya kujifungua na, kukamilisha mahudhurio ya Huduma za Kliniki wakati wa ujauzito, kukamilisha matibabu ya kifua kikuu na kuzuia sababu hatarishi na madhara yake. Pia, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea wamekuwa ni sehemu katika utekelezaji wa usimamizi jumuishi wa mikakati ya kudhibiti magonjwa ya watoto, jambo ambalo limefaulu kupunguza vifo vya watoto katika nchi zenye kipato cha chini na wastani.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuimarisha mfumo wake wa afya kwa kuhakikisha kuwa sehemu zote za mfumo wa afya zinaimarishwa, zinafanya kazi ipasavyo na kufikia kiwango cha utekelezaji unaokusudiwa. Kwa jumla, uimarishwaji wa Huduma ya Afya ya Msingi (PHC), ndio unaowahudumia watu wengi. Huduma za kinga na utoaji elimu ya Afya ni jambo la msingi ndani ya Huduma ya Afya ya Msingi. Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Mkakati wake wa Afya Zanzibar (ZCHS) imeamua kuanzisha Huduma za Afya ya Jamii katika ngazi ya Jamii (CBHP) ili kutoa huduma inayohitajika kwa wagonjwa au wateja wa huduma za afya ndani ya jamii wanayoishi.

Mkakati wa Afya ya jamii Zanzibar (ZCHS) unaelekeza kuwa utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya jamii utafanywa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs). Shirika la Afya Duniani (WHO) linatambua kada hii kuwa timu muhimu katika kuiwezesha jamii kusimamia masuala ya afya katika maeneo yao. Wahudumu hawa wamepewa jukumu la kuhakikisha kwamba lengo la kimkakati la ZCHS (2019-2025) la uimarishaji wa utoaji wa huduma endelevu za afya ya msingi zinayozingatia ushirikishwaji wa jamii, usawa na ufanisi kote Zanzibar limefanikiwa.

Hivyo, lengo mkakati la Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) litakuwa na thamani na kuweza kufikiwa kwa ufanisi iwapo utekelezaji wake utazingatia Afya jumuishi zilizoidhinishwa, sanifishwa na zilizoimarishwa katika mkakati huo utakao tekelezwa kupitia Wahudumu wa afya wa Jamii wa kujitolea. Mkakati huu wa Afya ya Jamii Zanzibar (ZCHS) (2019-2025) unahusu maeneo ya kimkakati yafuatayo:

- i. Kushajihisha na kutoa elimu ya afya kupitia mtu mmoja mmoja na kwa vikundi;
- ii. Kuchunguza viashiria vya hatari, vihatarishi, kukosa matembeleo au mahudhurio ya kupata huduma na tabia zisizofaa kwa ajili ya utekelezaji wa utoaji wa huduma katika programu mbalimbali zilizopangwa kutolewa katika ngazi ya jamii;
- iii. Kutoa rufaa kwenda kwenye vituo vya afya ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kuchunguza matatizo ya afya yaliyopo na kupeleka panapohusika ili kuweza kupata huduma stahiki za afya;
- iv. Usambazaji wa vifaa tiba na huduma za afya;
- v. Ukusanyaji wa taarifa katika jamii.

Shughuli hizi zinatakiwa kuwekwa katika programu za afya ambazo zitakuwa ni sehemu ya utowaji wa huduma katika ngazi za jamii ikiwemo Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana ambayo pia hujumuisha mambo muhimu kama vile Maendeleo ya Awali ya Watoto, Lishe, Kifua Kikuu, VVU, Malaria, mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona 2019 (UVIKO-19), maradhi yasiyopewa kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na ufuatiliaji wa usafi na mazingira.

1.2 Madhumuni ya utayarishaji wa Mwongozo wa Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea

Wazo la kutayarisha mwongozo wa Kiwango cha Huduma za Afya zinazopaswa kutolewa na wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) ulitokana muelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha huduma za afya za jamii zinaboreka zaidi na hatimaye kuzuia vifo vya mama na mtoto vinavyoweza kuepukika. Lakini hili pia limeshajihishwa na kuwezesha kutokana na utambuzi wa wadau muhimu katika mipango ya afya ya jamii Zanzibar. Kwamba kimsingi, mkakati wa afya ya jamii wa Zanzibar katika utekelezaji halisi hauwezi kupiga hatua bila kupatikana kwa miongozo sahihi ya afya na zana muhimu za kuwezesha utekelezaji wake.

Vivyo hivyo, Serikali inatambua na imeonekana kuwa utaratibu uliokuwepo wa kutekeleza huduma za afya za jamii kwa njia tofauti zilizogawanyika ambapo kila programu ya afya itajumuishwa katika shughuli za Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea kwa namna yake na kulingana na kila taasisi au idara inavyotaka bila kuwa jumuishi na inayofanana nchi nzima, hautasaidia kabisa kuimarisha matokeo au kuleta athari chanya inayotarajiwa na Serikali na wadau ambayo huwa inapatikana kwa kufanya kazi kwa pamoja na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) na kwa kufuata miongozo na vitendea kazi vilivyosanifishwa, vilivyo jumuishi, vilivyo boreshwa na vinavyofanana. Njia hizo tofauti na zisizojumuishi ambazo Mpango huu wa Afya ya Jamii Zanzibar (CBHP) unataka kuziondoa kwa kutumia hii miongozo mipya na vitendea kazi vipya vilivyotengenezwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau ni kama vile kutumia seti tofauti na miongozo binafsi ya utowaji wa huduma, utoaji wa mafunzo, utekelezaji, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini. Kwa kuongezea, wakati Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar unaweka misingi ya jumla kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Afya ya Jamii Zanzibar, vitendea kazi kama hivi na miongozo ya uhakika iliyopendekezwa kwenye mkakati haikuwepo kabla.

Katika majukumu yao ya utoaji huduma za afya za jamii katika ngazi ya jamii, Serikali, washirika wa utekelezaji, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) na wadau wengine wote watahitaji miongozo, itifaki na zana nyingine muhimu za kufanyia kazi. Vilevile, kuna umuhimu wa kuainisha na kuelekeza kazi na ujumla wa huduma ambazo Mhudumu wa Kujitolea katika Jamii na washirika wa utekelezaji kwa pamoja wanazopaswa na wanazoruhusiwa kuzitoa katika jamii. Kwa hivyo, ni mategemeo ya Serikali kwamba Mwongozo huu utatumika kama kitendea kazi na rasilimali ya kuleta mazingira wezeshi kwa kazi za Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea Zanzibar.

Hili neno "Kiwango cha utoaji wa Huduma za Afya" linamaanisha ni kiwango cha huduma ambacho kila Mhudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHV) anapaswa kutoa. Hiki ni kiwango cha chini kilichowekwa lakini kuna fursa ya ubunifu wa ziada kwa wadau wa Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) kuimarisha ufanisi na kupokea mikakati ya nyongeza wakati wa Utekelezaji baada ya kushauriana na kupata ruhusa kutoka serikalini.

1.3 Mpangilio na Matumizi ya Mwongozo wa Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya kwa Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea

1.3.1 Mpangilio wa Mwongozo

Mwongozo huu umepangwa katika sura tatu (3) ambazo zinafuatana kwa lengo la kumuwezesha mtumiaji kufahamu dhana ya kiwango cha huduma za afya zinazopaswa kutolewa kutoka sura ya kwanza kwenda sura nyingine. Kwa sababu hiyo, watumiaji wanatarajiwa kufuata mpangilio wa sura hizo ili kuelewa vizuri maudhui yaliyomo. Vilevile, wanaweza kuzitumia sura mbalimbali zenye kujitegemea, ambazo ni:

- Sura ya 1: inaonesha usuli na msingi wa uanzishwaji wa Mwongozo wa Kiwango cha Huduma za Afya na kuelezea kwa ufupi sura nyingine.
- Sura ya 2: inaeleza kwa ufupi maeneo ya programu kuu na miongozo ya Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea (CHVs).
- Sura ya 3: inafafanua kwa kina huduma na shughuli maalumu kwa kila eneo la programu iliyotajwa na kazi ambazo Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHV) wanatarajiwa kuzitekeleza kwa pamoja.

1.3.2 Walengwa wa Mwongozo Huu

Mwongozo huu unatarajiwa kutumiwa na wadau wote muhimu wa Mpango wa Afya ya Jamii Zanzibar ambao ni Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ na Wizara nyingine zinazohusiana na mipango ya afya katika ngazi ya jamii moja kwa moja. Pamoja na Watumiaji wengine wa programu za kiafya zilizo chini ya wizara ya afya, Washirika wa Maendeleo, Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu Vishiriki, Taasisi nyingine za Mafunzo na Elimu na Watekelezaji wengine ambao ni Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia, Asasi za Kijamii, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Jamii, Wakurugenzi wa Halmashauri, Timu za Usimamizi wa Afya za Wilaya, Watoa Huduma za Afya, Kamati za Ushauri za Shehia, Meya, Madiwani, Sheha, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea na Jamii kwa ujumla.

Wadau mbalimbali waliotajwa hapo juu watahiriki kikamilifu katika timu ya wataalamu wa utekelezaji wa Afya ya Jamii Zanzibar katika kuongoza shughuli za kila siku za kutekeleza Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP). *Kiambatisho 1* kinaeleza kwa kina kazi za Timu za Wataalam wa Afya ambazo zinatarajiwa kufanikisha shughuli za Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea Zanzibar kama sehemu muhimu ya Mpango wa Afya ya Jamii.

SURA YA 2

Maeneo ya Programu na Kiwango cha Utoaji wa Huduma za Afya katika Jamii kwa ajili ya Watoa Huduma ya Afya wa Kujitolea wa Jamii

2.1 Utangulizi

Mpango wa Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) unatoa miongozo katika mifumo mingi ya afya duniani. Kauli mbiu ya Afya kwa Wote ni "Mifumo na upatikanaji wa Huduma za Afya kwa jamii yote". Hii inamaanisha kuwa, huduma hazipaswi kutolewa kutokana na maoni ya watoa huduma au kutokana na mtazamo wa kitabibu lakini zitolewe kutokana na mitazamo na mahitaji ya mgonjwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya afya ya serikali. Kwa hivyo, siku zote tunapaswa kuwaweka wagonjwa na wateja karibu na huduma zilizopangwa kutolewa.

Wateja wetu ni miongoni mwa wanajamii. Jamii ina maanisha watu katika eneo fulani la kijiografia (kwa mfano Shehia) wenye mambo yanayofanana ikiwemo utamaduni na mashirikiano yao. Jamii zinaweza kushawishiana na kusababisha kuathiri utumiaji wa huduma za afya kwa mtazamo chanya au hasi. Kwa hivyo, ni muhimu wadau wote muhimu kama watekelezaji, wasimamizi, wakufunzi na watoa huduma wafahamu umuhimu wa kushirikisha jamii kikamilifu.

Hadi sasa, njia rahisi na bora za kudhibiti maradhi zinaleta matokeo ya chini kutokana na kutokuwepo na mgawanyo usio wa usawa wa huduma kwa jamii za chini kabisa vijijini. Kutokana na kasoro hizo, mfumo wa mabadiliko wa mikakati ya afya ya dunia umelenga kutoa huduma za msingi za afya kwa jamii kama ilivyopendekezwa na Mkutano wa Alma Ata mnamo 1978. Huduma ya Afya ya Msingi ilifafanuliwa na shirika la afya duniani kuwa, ni "huduma muhimu za afya zinazotakiwa zipatikane kila mahali kwa kila mtu hadi katika ngazi za kifamilia na kwa njia wanazokubaliana nazo kupitia ushiriki wao na kwa gharama nafuu".

Zanzibar inajulikana kuwa na historia ndefu ya utekelezaji mzuri wa Mpango wa Huduma ya Afya ya Jamii tangu mwazoni mwa miaka ya 1990. Tangu wakati huo, programu nyingi za Wizara zimekuwa zikitekelezwa kwa wakati mmoja na Wizara nyingine zilikuwa zikitekeleza kwa njia zao wenyewe kufikia malengo ya kijamii waliyoweka. Aidha, programu nyingi ziliibuka ikiwemo uanzishwaji kamati za afya, vilabu vya afya, kutawanywa wafanyakazi kwa jamii, watoa huduma wa nyumbani na Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea. Programu na miradi ilikuwa hapo awali inatekelezwa kwa matakwa ya programu husika na wakati mwingine huja na masharti ya kufadhili maeneo maalumu tu ya programu husika na kuacha mengine hata kama nayo ni muhimu. Jitihada za sasa kupitia mwongozo huu, ni kuwezesha na kuonesha njia za utekelezaji wa pamoja wa Programu za jamii kitaifa kwa njia jumuishi na endelevu.

Kwa hivyo, baada ya mashauriano na wadau wote muhimu wa usimamizi wa afya katika ngazi zote za kiserikali na kwa mwongozo ulioelezwa katika Mkakati wa Afya ya Jamii Zanzibar ZCHS (2019-2025), sehemu zifuatazo zinaeleza Kiwango kilichopangwa cha Utoaji wa Huduma za Afya (MIP) kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) kulingana na maeneo ya programu husika.

2.2 Programu na Afua zinazotekelezwa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea

Mkakati wa Afya ya Jamii ya Zanzibar (2019-2025) unabainisha na kuorodhesha majukumu na kazi muhimu zifuatazo za wahudumu wa Afya wa jamii kujitolea (Boksi 1):

Boksi 1: Kazi na majukumu ya Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (Chanzo: Mkakati wa afya ya jamii Zanzibar (ZCHS); 2019 - 2025)

Kuweka mahitaji kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya zilizopo na kuziimarisha kupitia mpango madhubuti wa uhamasishaji na elimu ya afya.

Uchunguzi na utambuzi wa dalili za hatari, vihatarishi, ukiukwaji wa taratibu za mahudhurio ya kupata huduma, tabia zisizofaa na matatizo yanayoambatana na ujauzito.

Utoaji wa mafunzo na ushauri kwa mtu mmoja mmoja na vikundi.

Utoaji wa huduma za rufaa katika vituo

Ufuatiliaji wa kero zinazojitokeza, huduma za rufaaa kwa vituo vya afya na jamii.

Uchunguzi wa awali kwa kutumia vipimo vya haraka.

Vipaumbele vya matembeleo ya kaya na kutoa huduma au uelimishaji kwa kuzingatia mahitaji mahsusi ya Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana, hasa miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kuweza kupata ujauzito (WRA).

Majukumu na kazi hizi yanaweka msingi wa kufafanua mikakati muhimu itakayotekelezwa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. Vilevile, inaweka msingi wa kuwasaidia kutoa huduma katika ngazi ya jamii. Sehemu zifuatazo zinaeleza Afua na programu zitakazotekelezwa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea kupitia majukumu na kazi zilizotajwa hapo juu. Ikimaanisha kwamba, kila programu ya afya iliyopo ambayo wataitumia Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. Programu hizo zitatekelezwa kulingana na kazi na majukumu ya Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea yaliyotajwa hapo juu.

2.2.1 Afua namba 1: Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana (RMNCAH)

Kifupisho cha RMNCAH ni Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana. Kila kipengele kimoja cha mkakati huu kinajumuisha matokeo muhimu ya kila eneo katika kielelezo cha Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana, na kila eneo maalumu la kimkakati lililotajwa. Huduma hiyo ni mwendelezo wa matokeo ya maeneo yaliyoelezwa katika mikakati iliyomo ambayo inapaswa kuthaminiwa kutoka sasa na baadaye. Mwendelezo huu unahitajika ili kufikia ufanisi wa utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Hata hivyo, kuna huduma maalumu ambazo hutolewa katika vituo vya huduma vilivyobobea ambapo wataalamu na washauri wanapatikana. Kwa mfano, katika hospitali za mikoa na taifa. Hata hivyo, ubobezi na utaalumu kwa watoa huduma za Afya huwa unapungua kadri unaposhuka katika ngazi za chini za utoaji wa huduma za afya. Hivyo, katika ngazi ya jamii utaalumu na ubobezi unakosekana kabisa. Kwahiyo, watoa huduma na wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea (CHVs) wanatakiwa kujifunza na kuelewa kuhusu utoaji sahihi wa huduma zote katika Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana. Hii inaashiria umuhimu huu wa kuchagua kwa uangalifu Afua na Huduma mbalimbali zitakazotolewa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. Ni wazi kuwa ni muhimu kuwa na Kiwango maalumu cha utoaji wa huduma kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) kama ilivyoainishwa waziwazi katika mwongozo huu.

Kwa kuzingatia mapendekezo ya wadau na kama ilivyoelekezwa na Mkakati wa Afya ya Jamii ya Zanzibar (ZCHS 2019 - 2025), programu zifuatazo za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana zilipendekezwa zijumuishwe katika Mwongozo wa kiwango cha utoaji wa huduma kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea Zanzibar (Jedwali 1).

Jedwali 1: Kiwango cha huduma za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana

Kipengele cha RMNCAH	S#	Maeneo Muhimu ya Programu
Afya ya Uzazi	1	Uzazi wa mpango unaofaa wa kutoa nafasi ya kusubiri au kufunga uzazi
	2	Saratani zinazohusiana na Afya ya Uzazi
	3	Ushiriki wa kijinsia akiwemo mwanamme
	4	Programu ya huduma za uzeeni zilizomo katika Afya ya uzazi, mama, mtoto na vijana
Afya ya Mama	1	Huduma za kliniki kwa mama wajawazito (ushauri, uangalizi na kutayarishwa kabla ya kujifungua)
	2	Huduma za rufaa zenye ufanisi na zilizotimia
	3	Vifaa tiba vya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto
	4	Utambuzi wa mama wajawazito na kujiandaa mapema katika Utoaji wa Huduma za kliniki kwa mama wajawazito
	5	Kuzuia Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto
	6	Kujifungua katika vituo vya afya au taasisi zinazotoa huduma za uzazi
	7	Huduma baada ya kujifungua
	8	Uzazi wa Mpango baada ya Kujifungua
	9	Huduma baada ya Mimba kuharibika
	10	Kuzuia na kudhibiti maambukizi ikiwa ni pamoja na elimu katika kaya juu ya maambukizi ya UVIKO 19
	11	Utoaji elimu ya lische kwa mama baada ya kujifungua

Afya ya Mtoto anayezaliwa	1	Unyonyeshaji wa haraka baada ya kujifungua
	2	Unyonyeshaji kwa muda wa miezi sita mfululizo bila kuwapa watoto wachanga vyakula vingine
	3	Usafi wa mtoto.
	4	Usimamizi wa watoto waliokuwa hawajatimia miezi tisa ya mimba (njiti) na wenye uzito mdogo
	5	Usimamizi wa watoto wachanga walio wagonjwa
Afya ya Mtoto	1	Makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto
	2	Uthibitiwa maradhi sugu ya watoto
	3	Utaratibu wa kupata chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano ikiwepo vitamini A
	4	Kujenga tabia ya kunyonyesha
	5	Unyonyeshaji wa watoto na utaratibu mzuri wa lishe.
	6	Uthibiti wa utapiamlo mkali
	7	Taratibu na matendo sahihi katika kaya na Jamii
Afya katika umri wa kubalehe	1	Huduma Rafiki za uzazi kwa vijana
	2	Ujuzi, maarifa juu ya ujinsia na afya ya uzazi.
Ukaguzi wa vifo vya uzazi mama na mtoto	1	Ufuatiliaji na kukabiliana na hatari za vifo vya Mama na Mtoto baada ya kujifungua

2.2.2 Afua namba 2: Lishe

Zifuatazo ni programu na mikakati inayojumuishwa katika Afua ya upatikanaji lishe (Jedwali 2):

Jedwali 2: Orodha ya programu na mambo yaliyomo katika Afua ya upatikanaji wa lishe

Kipindi		Mambo muhimu ya Kuzingatia
Kipindi cha ujauzito	1	Lishe bora wakati wa ujauzito na elimu juu ya unyonyeshaji
	2	Upatikanaji wa lishe bora na mlo kamili
Baada ya kujifungua	33	Kuanza mapema unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mfululizo kwa muda wa miezi sita bila kuchanganya na vyakula vingine
	1	Kutambua matatizo ya ulaji na ukuaji wa mtoto
	2	Ulishaji kwa watoto waliozaliwa na uzito mdogo pamoja na watoto njiti
Mtoto mchanga na watoto	1	Utambuzi wa mapema na rufaa ya utapiamlo (ikiwemo kipimo cha uchunguzi wa utapiamlo cha begani na ufuatiliaji katika kaya kwa ukuaji wa mtoto)
	2	Kiwango cha wastani cha chakula bora kitakacho imarisha lishe, hali ya unyonyeshaji na vyakula mchanganyiko
	3	Virutubisho vya nyongeza (unga wa lishe kwa watoto baada ya miezi 6; watoto na pia kwa mama miezi 3 baada ya kujifungua)

2.2.3 Afua namba 3: Kifua Kikuu/VVU na UKIMWI

Afua ya Kifua Kikuu/VVU na UKIMWI inafuata hatua zifuatazo (Jedwali 3):

Jedwali 3: Orodha ya Mikakati inayofaa kuchukuliwa katika programu za Kifua Kikuu /VVU na UKIMWI

Vitengo		Mkakati
Kitengo cha jamii kinachojihusi sha na Kifua	1	Utafutaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu kwenye jamii na kuwapatia rufaa
	2	Kukusanya na kusafirisha makohozi
	3	Msaada wa matibabu
	4	Kufuatilia wagonjwa waliopotea na kukiuka hatua za matibabu

Kikuu	5	Ufuatiliaji wa watu wanaoishi pamoja na wagonjwa waliothibitishwa kuwa na bacteria wa kifua kikuu
	6	Elimu ya afya na ushauri nasaha
	7	Kuzuia na kudhibiti maambukizo
Kitengo cha jamii kinachojihusi sha na VVU na UKIMWI	1	Utunzaji wa wagonjwa mahututi majumbani
	2	Ufuatiliaji wa wagonjwa walioacha taratibu za mahudhurio ya matibabu
	3	Elimu ya afya na ushauri nasaha
	4	Msaada wa matibabu

2.2.4 Afua namba 4: Malaria

Programu ya malaria katika ngazi ya jamii itajumuisha yafuatayo:

Jedwali 4: Orodha ya mikakati ya programu ya Malaria

Shughuli		Mkakati
Shughuli za kuzuia Malaria	1	Malaria wakati wa ujauzito
	2	Kudhibiti mbu wanaosambaza malaria (Matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu) na udhibiti wa vidimbwi vya kuzalisha mbu na upuliziaji wa dawa za kuulia mbu.
	3	Ubadilishaji wa jumla wa tabia za jamii

2.2.5 Afua namba 5: Afya ya Mazingira, Maji na Usafi

Mikakati mbalimbali chini ya Afua hii unahusisha mambo yafuatayo hapo chini.

Jedwali 5: Orodha ya Mikakati mbalimbali chini ya Afua ya usafi wa Maji, Afya ya Mwili na Usafi wa Mazingira

Shughuli		Mikakati
Usafi wa Mazingira	1	Kuzuia uchafuzi wa maji na hewa ili kuwa na maji safi
	2	Ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji ili kudumisha wingi wa maji
Maji, Afya ya Mwili na Mazingira	1	Usafi na Usalama na kuwepo kwa sheria na kanuni za usalama wa chakula
	2	Usafi wa kuosha mikono kwa sabuni au vitakasa mikono vingine (baada ya kujisaidia, kutupa kinyesi cha watoto, nepi, na kabla ya kuandaa, kula na kushughulikia chakula)
	3	Kuhamasisha usafi wa mazingira ili kutunza na kuimarisha utupaji wa taka
	4	Usimamizi wa taka ngumu na za majimaji

2.2.6 Afua namba 6: Maradhi Yasiyoambukiza

Maradhi yasiyo ya kuambukiza yanaongezeka sana duniani na Zanzibar haiwezi kujitenga katika kadhia hii mpya ya ulimwengu. Sababu za kawaida za maradhi yasiyo ya kuambukiza (NCD) zinahusishwa na mitindo ya maisha na namna ya ulaji na pia urithi wa kimaumbile na kibaologia. Hatua za kupambana na maradhi yasiyo ya kuambukiza (NCD) zinatolewa katika vituo vya afya. Hata hivyo, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea (CHVs) katika ngazi ya Jamii wanatarajiwa kushiriki katika utekelezaji wa mikakati iliyomo katika Jedwali la 6 ili kusaidia kupunguza maradhi ya kuambukiza Zanzibar.

Jedwali 6: Mikakati inayofaa kuchukuliwa dhidi ya Maradhi Yasiyoambukiza

Aina		Mikakati
Kwa Watoto wachanga	1	Unyonyeshaji wa miezi 6 mfululizo bila kuchanganya na vyakula vingine
	2	Lishe ya kutosha na unyonyeshaji wa mara kwa mara
	3	Unyonyeshaji mpaka miaka miwili au zaidi
Kwa watoto wadogo na vijana	1	Elimu ya mfumo wa maisha
	2	Shughuli za mazoezi ya mwili skuli na katika jamii
	3	Ajali za barabarani
	4	Vyakula salama na vyenye afya shuleni
	5	Kuzuia uuzaji na utumiaji wa bidhaa za chakula zenye chumvi

		nyingi/sukari/mafuta yasiyofaa
Watu wazima	1	Lishe ya mama
	2	Programu za kuzuia na kukomesha tumbaku
	3	Upatikanaji wa chakula bora cha kutosha
	4	Mazoezi ya mwili (sehemu za kazi na sehemu maalumu)
	5	Njia sahihi za kuzuia vihatarishi, Maradhi na madhara yatokanayo na maradhi

2.2.7 Afua namba 7: Magonjwa Yasiopewa Kipaumbele

Shirika la Afya Duniani linapendekeza hatua zifuatazo za kuzuia na kudhibiti Maradhi yasiopewa Kipaumbele. Mikakati hii inaweza kutekelezwa katika mifumo ya afya ya ngazi zote ikiwemo ya kijamii. Huduma mbalimbali ambazo Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea za (CHVs) wanaweza kuzitoa kwa jamii kwenye kila moja ya mikakati hii itafafanuliwa katika sura ya tatu. Mikakati hiyo inajumuisha mambo yafuatayo:

Jedwali 7: Mikakati ya magonjwa yasiopewa kipaumbele

Mkakati	Maelezo
Njia za kuzuia maradhi	Hii pia inahusu sana kutabua na kuzuia maradhi ambayo ni vigumu kugundulika mapema na wakati mwingine yanapokuwa yamecheleweshwa kugundulika yanaleta madhara makubwa ya Afya. Njia hizi zinatumika katika ngazi ya kaya ili kuweza kuzuia maradhi mbalimbali
Udhibiti wa maradhi yanayosambazwa na wadudu	Inajumuisha usalama wa usimamizi wa kutumia viuatilifu katika mazingira ya kijamii katika kudhibiti usambazwaji wa maradhi kwa njia ya wadudu kupitia utaratibu wa kudhibiti maradhi yanayosababishwa na wadudu. Upulizaji wa dawa za kuulia mbu na mazalia yake ni mfano mzuri
Maji safi na salama huduma za msingi za usafi wa mazingira na usafi wa mwili pamoja na elimu	Hii inahusiana na mpango wa usafi wa Maji, Afya ya Mwili na usafi wa Mazingira.
Mabadiliko ya mfumo wa mawasiliano kijamii na kitabia kwa kushughulikia Maradhi yasiopewa kipaumbele	Huduma Iliyoambatana na uanzishwaji wa mpango wa Mabadiliko ya mfumo wa mawasiliano kijamii na kitabia pamoja na programu zilizobaki.
Utoaji wa dawa za kijikinga na maradhi (minyoo, matende n.k)	Mara nyingi kupitia kampeni za kitaifa na kuungwa mkono kupitia shughuli za kijamii.

2.2.8 Afua Namba 8: Ufuatiliaji na Tathmini

Mikakati katika eneo hili itajumuisha:

Mkakati	Maelezo
Mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii	Mfumo unaotakiwa kufanya kazi yake katika ngazi ya chini Kabisa. Yaani CHIS.
Data na takwimu	Kukusanya takwimu za Jamii, kuzichanganua kwa mfumo wa kidigitali na kuzihifadhi katika Mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii (CHIS)
Matumizi ya	Kuweka takwimu katika muonekano mzuri na Kutumia taarifa kwa

Takwimu	msaada wa wasimamizi
Kuripoti	Kutoa ripoti za kazi kama ilivyoelekezwa na wasimamizi

2.2.9 Afua Mtambuka

Katika eneo hili, mambo yafuatayo yatajumuishwa:

- Uongozi na utawala
- Mpango shirikishi wa afya
- Uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali
- Huduma za kuhuisha afya, na
- Ufuatiliaji wa taarifa za magonjwa na afya ya Jamii.

SURA YA 3

Kiwango cha Utoaji wa Huduma kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea huduma mbalimbali zinazotolewa na wahudumu wa afya wa jamii wa kujitolea (CHVs) ambazo zinajumuishwa kutokana na maeneo saba ya utoaji wa huduma kama ifuatavyo:

- 1) Kuweka mahitaji kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya zilizopo na kuziimarisha kupitia mpango madhubuti wa uhamasishaji na elimu ya afya
- 2) Uchunguzi na utambuzi wa dalili za hatari, vihatarishi, ukiukwaji wa taratibu za mahudhuro za kupata huduma, tabia zisizofaa na matatizo yanayoambatana na ujauzito
- 3) Utoaji wa mafunzo na ushauri kwa mtu mmoja mmoja na vikundi
- 4) Utoaji wa huduma za rufaa katika vituo vya afya
- 5) Ufuatiliaji wa kero zinazojitokeza, huduma za rufaaa kwa vituo vya afya na jamii.
- 6) Uchunguzi wa awali kwa kutumia vipimo vya haraka
- 7) Vipaumbele vya matembeleo ya kaya na kutoa huduma kuzingatia mahitaji mahususi ya Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana, hasa kwa wanawake walio katika Umri wa kuweza kupata ujauzito.

Sehemu inayofuata hapo chini inaonyesha aina ya huduma hizi kuu saba ambazo zitatekelezwa kwenye kila moja ya Afua.

3.2 Huduma zitakazotolewa kwa kila Afua

3.2.1 Afua namba 1: Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana

Huduma mbalimbali zinazotolewa kwa ajili ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto zinaelezwa katika jedwali la 8 lifuatalo:

Jedwali 8: Mkakati wa Utoaji wa Huduma kwa Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana

Eneo	Afua	Huduma itakayotolewa na wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea (CHV)
Afya ya uzazi	Uzazi Mpango Wa	Kuendeleza mpango thabiti wa uzazi wa mpango na huduma za kiafya katika Shehia, kufanya sensa za watu ili kujua ongezeko la watu Kutoa Elimu ya Uzazi wa Mpango Kuanzia Ngazi ya Kaya Kufanya mikutano na wazee, vijana wa kike na wa kiume na wazee wa vijiji Kuwa na mfumo maalumu wa ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani. Kuhakiki, kuwajumuisha na kuwashirikisha watu wote Kuhakiki rufaa za wagonjwa Kutunza kumbukumbu za huduma za uzazi wa mpango katika maeneo mahususi
	Kansa Kizazi Ya	Kutoa elimu na ushauri juu ya kansa ya kizazi Rufaa kwa wagonjwa wa kansa ya kizazi
	Jinsia, , Ushirikishwaji wa mwanamme pamoja na udhalilishaji wa Kijinsia	Kuhamasisha jamii kutoka ngazi ya familia, jamii na mikutanoni umuhimu wa kuwashirikisha wanaume katika afya ya uzazi kama uzazi wa mpango, kuanza huduma za kupima ujauzito mapema na kujifungua katika kituo cha afya Kutoa elimu inayohusu upunguzaji wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ili kuboresha afya ya uzazi

	Huduma kwa wazee kupitia programu ya afya ya mama na mtoto	Kutoa taarifa kamili zinazohusu elimu ya uzazi kwa wazee Kuweka wazi viashiria vya maradhi yasiyoambukiza na dalili za maradhi hayo.
Hudu ma kwa mama	Huduma ya kliniki kupima ujauzito	Usafi wa mtu binafsi na tabia zenye kujenga afya Utambuzi wa mapema wa ujauzito katika ngazi ya jamii Ugunduzi mapema dalili za hatari Kuhamasisha kuanza mapema kupima ujauzito na kuanza kliniki ya mama wajawazito ndani ya miezi 3 ya kwanza ya ujauzito na pia kuhakikisha kliniki zote za ujauzito zinakamilika kama inavyotakikana Kuhamasisha kujifungulia katika kituo cha afya ili kuepuka hatari kubwa inayotokana na kujifungulia majumbani Kuelimisha umuhimu wa matayarisho na maandalizi ya kujifungua Kuelimisha wanajamii kuhusu dalili za hatari wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua Kushajihisha tabia za kiafya wakati wa ujauzito hususani usafi binafsi, ushauri wa kufanya mazoezina mlo kamili wakati wa ujauzito Kuelimisha jamii madhara na hatari ya kutumia dawa za kienyeji Kuelimisha wanajamii uwezekano wa kina wa huduma baada ya kuharibika mimba kwa usalama
	Rufaa	Kutambua mapema na kutoa rufaa ya matatizo ya ujauzito Kuwezesha rufaa ya matatizo yanayojitokeza wakati wa ujauzito, kujifungua na baada ya kujifungua iwapo amejifungulia nyumbani Ufuatiliaji wa kina kuhakikisha huduma za rufaa zina ufanisi na ni zenye kukamilika
	Usambazaji wa vifaa na dawa kwa ajili ya Afya ya mama na Mtoto	Kuhamasisha matumizi sahihi ya dawa zilizopendekezwa wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua katika ngazi ya jamii Kusambaza baadhi ya vifaa na dawa zilizopendekezwa kwa kina mama wanaohitajika (kama vile matumizi ya ferasi na vifaa vyengine vya uzazi wa mpango) katika jamii Fuatilia na tambua upungufu wa vifaa na dawa na kufuatilia mbadala sahihi
	Kuzuia Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto HIV / Homa ya ini B na C	Kuhusisha wanandoa na wanaoishi pamoja wenye VVU/AIDS, homa ya ini B na C kuzuia maambulizi yanayotoka kwa mama kwenda kwa mtoto kuweza kupata huduma katika kituo cha afya kilicho karibu nao Kufuatilia wagonjwa waliokiuka taratibu za matibabu kwa ajili ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto Kutoa elimu na ushauri kuhusu kuzuia maambukizi kwa watoto ambao wamezaliwa na wenye virusi vya Ukimwi
	Uangalizi baada ya kujifungua	Kuelimisha na kuhamasisha wagonjwa na jamii kwa ujumla juu ya: Kuanza kunyonyesha mapema na kwa mfululizo bila kuchnganya na vyakula vingine Huduma baada ya kujifungua kwa mama na mtoto kwa muda wa siku 42 Kutoa elimu ya utambuzi wa mapema wa dalili hatarishi baada ya kujifungua na kupatiwa huduma za rufaa Uangalizi maalum wa watoto wachanga (wenye uzito mdogo na watoto njiti) Tabia za kujenga afya (kama vile kufanya mazoezi na usafi wa mwili)

		<p>Uzazi wa mpango baada ya Kujifungua (PPFP) Chanjo kwa watoto chini ya miaka 5 Kutumia chandarua kilichotiwa dawa ya viuatilifu Lishe ya mama baada ya kujifungua</p>
Afya ya mtoto mchanga	Huduma za Muhimu kwa watoto wachanga	<p>Kuhamasisha unyonyeshaji wa watoto mapema baada ya kuzaliwa kwenye mikutano au unapowatembelea nyumbani Kuelimisha usafi kwa mtoto Kuelimisha utunzaji na usafi wa kitovu kwa mtoto mchanga Kuelimisha namna ya kumpatia huduma mtoto aliezaliwa kabla (njiti)na wenye uzito mdogo Kuelimisha namna ya kutambua mapema dalili za hatari kwa watoto wachanga na kuwapatia rufaa</p>
Afya ya Mtoto	Makuzi ya awali ya mtoto	<p>Kuelimisha jamii katika kaya na kwenye jamii juu ya dhana ya makuzi ya awali ya mtoto Hamasisha unyonyeshaji wa mapema mara tu baada ya kujifungua Kutambua na kusaidia msongo wa mawazo na tishio linaloweza kudhuru ukuaji wa mtoto wakati wa ujauzito Kuhamasisha na kutoa mafunzo kuhusu mambo yafuatayo; Kutoa hamasa ya mapema kwa mama mjamzito itakayomsaidia kuimarisha afya yake wakati wa ujauzito Kutoa hamasa inayosaidia kuimarisha afya ya mtoto mchanga Ukaribu baina ya mtoto na mzazi Usalama, na kuwawezesha Uhusiano wenye tija, na ushirikishwaji wa wanaume katika malezi Ushirikishwaji Uwajibikaji wa pamoja katika malezi bora Kubaini viashiria vya hatari kwa maendeleo ya mtoto (mf. Kuangalia maendeleo ya ukuaji, kupata msongo wa mawazo, ulizi wa mtoto, nidhamu, kupuza kwa mtoto na kunyanyaswa /kudhalilishwa kwa mtoto)</p>
	Matibabu ya maradhi muhimu ya watoto	<p>Uelimishaji wa jamii jinsi ya kutumia ORS na madini ya zinki kwa uangalizi wa nyumbani kwa maradhi ya kuharisha na kutoa huduma ya rufaa kwa mtoto anayeharisha kwa muda mrefu Kutambua, kusimamia na kudhibiti ugonjwa na kumpatia huduma ya rufaa kwa homa kali</p>
	Utoaji wa chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano (na chanjo za nyongezaza na Vitamini A)	<p>Kuelimisha, kuhamasisha na kuunga mkono kampeni na shughuli za utoaji chanjo Kushiriki na kusaidia katika shughuli za ziada za chanjo (SIAs) na kampeni za kutoa matone ya VitaminiA Kufuatilia na kubaini watoto na kina mama wanaokiuka taratibu za chanjo na kuwarudisha tena kwenye huduma ya chanjo katika vituo vya afya vilivyo karibu nao Kuweka rekodi ya wanaokiuka taratibu za chanjo na kuwahamasisha walioko majumbani na kumuunganisha na rekodi zilizopo katika kituo cha afya na hatimae kwenye mfumo taarifa za afya ya jamii.</p>
Afya ya vijana	Huduma Rafiki kwa Vijana ikiwemo Afya ya Uzazi pamoja huduma za VVU	<p>Kutoa elimu kwa vijana wenye umri wa balehe kuanzia umri 10-19 na vijana wa umri wa kati miaka 24 juu ya afya ya uzazi, ngono salama na elimu ya chanjo kwa mtu mmoja mmoja au kwa kikundi Kuwaunganisha na kuwahamasisha upatikanaji wa huduma katika vituo vilivyo karibu nao vinavyotoa huduma za afya ya uzazi salama. Kuwashauri na kuwapeleka vijana kwa kupata huduma na upimaji wa VVU Kukuza na kuwashauri vijana wa kike kuhusu chanjo ya virusi vya</p>

		papilloma (HPV)
	Ujuzi, uzoefu na tabia nzuri juu ya ujinsia na afya ya uzazi	Kuelimisha, kuhamasisha na kuwasisitiza vijana juu ya matendo, tabia nzuri katika mahusiano ya ngono
Ukaguzi na ufuatiliaji wa vifo mama na mtoto	Ufuatiliaji na kukabiliana na vifo vya mama na mtoto	Kushiriki katika ufuatiliaji na kukabiliana na vifo vya mama na mtoto

3.2.2 Afua namba 2: Lishe

Lishe ni mada mtambuka ambayo imejitokeza katika Afua nyingine ambayo ni muhimu katika afya ya uzazi, mama, mtoto na Vijana. Hii pia imejadiliwa katika Afua ya maradhi yasiyo ya kuambukiza, ingawaje baadhi ya maelezo ya kina yameelezwa katika seti nyingine kutokana na umuhimu wake na baadhi ya vipengele vyake muhimu vimechanganywa pamoja hapa kwa ajili ya kurahisisha usomaji na kuviweka katika seti ya pamoja.

Hivyo, Mpango huu utajumuisha Afua ya lishe.

Jedwali 9: Orodha ya hatua, mikakati na huduma zilizomo katika Afua ya lishe

Hatua	Mikakati	Huduma itakayotolewa na wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea (CHV)
Wakati wa ujauzito	Lishe bora wakati wa ujauzito na unyonyeshaji	Kuelimisha, kuhamasisha na kukuza lishe yenye afya wakati wa ujauzito na unyonyeshaji kulingana na chakula chenye lishe bora kinachopatikana katika jamii Ugawaji wa virutubisho vya nyongeza kama itakavyoshauriwa
Baada ya kujifungua	Namna nzuri ya unyonyeshaji	Kuelimisha na kuhamasisha umuhimu wa kuanza mapema kunyonyesha Kutambua matatizo ya ulaji na ukuaji. Upatikanaji wa lishe bora na mlo kamili. Ulishaji kwa watoto waliozaliwa na uzito mdogo pamoja na watoto njiti.
Kipindi cha utoto	Namna ya ulishaji kwa watoto wachanga	Utambuzi wa mapema na rufaa ya utapiamlo (ikiwemo kipimo cha uchunguzi wa utapiamlo na ufuatiliaji wa nyumbani wa ukuaji wa mtoto) Kiwango cha wastani cha chakula bora kitakacho imarisha lishe, hali ya unyonyeshaji na vyakula mchanganyiko. Virutubisho vya nyongeza (unga wa lishe kwa watoto baada ya miezi 6; watoto na pia kwa mama miezi 3 baada ya kujifungua)
Jamii kwa ujumla	Tabia za ulaji na mlo kamili	Kuwapatia elimu na mapendekezo kiasi cha lishe kinachokubalika katika jamii kwa ujumla, vijana, wazee na watu wenye magonjwa sugu.
Kwa wazee	Lishe bora kwa wazee	Kuhamasisha matumizi ya mlo kamili kwa ajili ya kukamilisha lishe (ikiwemo unyonyeshaji wa lazima na vyakula mbalimbali).
Kwa watu wenye maradhi sugu	Lishe kwa watu wenye maradhi sugu	

3.2.3 Afua namba 3: Kifua Kikuu (TB), VVU na UKIMWI

Mpango wa TB/VVU na UKIMWI utatekezwa kwa kufuata mikakati ifuatayo (Jedwali 10):

Jedwali 10: Orodha ya Mikakati inayofaa kuchukuliwa katika Afua ya Kifua Kikuu/VVU na UKIMWI

Kitengo	Mkakati	Huduma itakayotolewa na wahudumu wa Afya wa Jamii wa kujitolea (CHV)
Shughuli za huduma za kifua kikuu katika jamii	Kuchunguza ugonjwa wa Kifua Kikuu katika jamii na kupatiwa huduma za rufaa.	Kuchunguza ugonjwa wa Kifua Kikuu katika jamii na kupatiwa huduma za rufaa.
	Ukusanyaji, usafirishaji na uhifadhi wa makohozi.	Kusaidia katika ukusanyaji, usafirishaji na uhifadhi wa makohozi kutoka katika jamii.
	Msaada wa matibabu	Kutoa msaada kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu waliopo nyumbani kulingana na miongozo ya kitaifa
	Ufuatiliaji wa wagonjwa walioacha taratibu za mahudhurio ya matibabu.	Kuandaa na kuweka utaratibu wa rekodi ya wanaokiuka taratibu za chanjo na kuwahamasisha wenye magonjwa majumbani kwa kuweka rekodi ili kujumuishwa katika vituo vya afya.
	Elimu ya afya na ushauri nasaha	Kutoa elimu ya afya (ikiwemo uhibititi, kujikinga na kuzuia) na kutoa ushauri juu ya kifua kikuu kwa ujumla miongoni mwa jamii ndani ya eneo lako.
Huduma zinazohus u VVU na UKIMWI katika jamii	Huduma za wa wagonjwa majumbani kwa wale wanoumwa sana.	Kufanya ziara za mara kwa mara kwa wagonjwa mahututi na kuelekeza huduma inayopendekezwa kulingana na miongozo ya kitaifa.
	Ufuatiliaji wa wagonjwa walioacha taratibu za mahudhurio ya matibabu.	Ufuatiliaji wa wagonjwa walioacha taratibu za mahudhurio ya matibabu na waunganishe katika kituo cha karibu
	Elimu ya afya na ushauri nasaha	Kutoa elimu ya afya na ushauri juu ya VVU na UKIMWI kwenye jamii iliopo katika maeneo yako
	Msaada wa matibabu	Kufanya matembeleo katika kaya na kutoa huduma kulingana na miongozo ya kitaifa ikiwa ni pamoja na kuwapelekea dawa wanazotumia za kupunguza makali ya virusi ARVs ikiwepo wagonjwa wanaondelea vizuri (hawana matatizo)

3.2.4 Afua namba 4: Malaria

Baadhi ya huduma na afua kama vile elimu juu ya Malaria wakati wa ujauzito na utumiaji wa vyandarua vilivyowekewa dawa ya muda mrefu zimejumuishwa katika programu zingine kama Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana. Hata hivyo, kwa ajili ya uelewa wa Malaria katika sehemu hii, zifuatazo ni huduma za msingi na muhimu kwa ajili ya mikakati ya programu ya malaria (jedwali 11):

Jedwali 11: Mikakati ya kijamii kwa ajili ya Programu za malaria

Mkakati	Huduma zinazotolewa na wahudumu wa afya wa jamii wa kujitolea.
Malaria wakati wa ujauzito	Kufanya ziara majumbani na kutoa elimu kupitia mikutano inayohusu malaria na hatari zake wakati wa ujauzito
Matumizi ya vyandarua vyenye dawa ya kudumu (LLIN)	kutoa elimu kuhusu Malaria kwa ujumla (sababu, madhara ya malaria, njia ya maambukizi) na mikakati yakujikinga ikiwemo matumizi ya (chandarua chenye dawa ya kudumu) Kushiriki katika usambazaji wa vyandarua vyenye dawa ya kudumu Kufuatilia matumizi ya vyandarua vyenye dawa katika kiwango cha kaya na katika jamii kwa ujumla

Kutunza usafi wa mazingira na mazalia ya mbu yaliopo nje ya nyumba	Kuelimisha, kuhamasisha na kuendeleza utunzaji wa mazingira ikiwa ni mbinu ya kuzuia ueneaji wa malaria Kushirikiana na kamati ya afya kiongozi ya Shehia kuhamasisha na kushajihisha siku maalumu ya utunzaji ya usafi wa mazingira Shiriki katika kampeni za dawa za kuulia mbu na wadudu wengine nje ya nyumba
Mabadiliko ya mfumo wa mawasiliano na kitabia katika jamii	Tumia miongozo ya Mabadiliko ya mfumo wa mawasiliano kijamii na kitabia kama ilivyoelekezwa na miongozo ya kitaifa

3.2.5 Afua namba 5: Afya ya Mazingira, Maji na Usafi

Jedwali la 12 hapa chini linaelezea mfumo wa huduma wa Usafi wa Maji, Afya ya Mwili na Mazingira.

Jedwali 12: Mikakati ya kijamii kwa ajili ya usafi wa Maji, Afya ya Mwili na Mazingira

Mikakati	Huduma zinazotolewa na wahudumu wa afya wa jamii wa kujitolea.
Kuzuia uchafuzi wa maji na hewa ili kuongeza uwepo mzuri na maji;	Kutoa elimu na kuhamasisha uhifadhi wa mazingira ili kulinda vyanzo vya maji kwa ujumla Kutoa elimu ya Afya ya Mazingira na usafi wa Maji, Mwili na vitu vyao binafsi Kuhamasisha mabadiliko ya kitabia yanayohusiana na Afya ya Mazingira na usafi wa Maji na Mwili juu ya matumizi ya maji safi na salama, ujenzi na matumizi ya vyoo na kuosha mikono kwa sabuni na maji tiririka. Kuweka kumbukumbu ya kaya zenye maji safi na salama Kuweka kumbukumbu ya nyumba zinazotumia vyoo Kuelisha jamii juu ya usalama na afya ya chakula na bidhaa zinazohusiana nazo zijulishe mamlaka za serikali juu ya kuenea kwa chakula na bidhaa nyingine zenye kutiliwa mashaka kuhusu ubora na usalama wake
Ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji ili kudumisha wingi wa maji;	
Usafi na Usalama na kuwepo kwa sheria na kanuni za usalama wa Chakula.	
Usafi wa kuosha mikono kwa sabuni au vitakasa mikono vingine (baada ya kujisaidia, na kabla ya kuandaa, kula na kushughulikia chakula na namna ya kutupa kinyesi cha watoto, nepi,) na	
Kuhamasisha usafi wa mazingira ili kutunza na kuimarisha utupaji wa taka.	

3.2.6 Afua namba 6: Maradhi Yasiyo ya Kuambukiza

Maelezo yafuatayo yanahusu utoaji wa huduma kwa Maradhi yasiyo ya kuambukiza. (Jedwali 13)

Jedwali 13: Hatua za afya ya jamii kuhusu Maradhi yasiyo ya Kuambukiza

Hatua	Mkakati	Huduma zinazotolewa na wahudumu wa afya wa jamii wa kujitolea.
Mtoto mchanga	unyonyeshaji wa miezi sita mfululizo	Kuunganisha Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na programu za lishe.
	Upatikanaji wa lishe na mlo wa ziada	
	Afya ya uzazi wa Mama na Mtoto	
Watoto na Vijana	Mawasiliano na mabadiliko ya kijamii	Kutoa elimu ya stadi za maisha
		Kwa kushirikiana na Kamati kiongozi za Afya katika Shehia. Kutoa elimu na kuhamasisha, Shughuli za mazoezi ya mwili kwenye skuli na katika jamii.

		Kwa kushirikiana na Kamati kiogozi za Afya katika Shehia na maofisa wa elimu kutoka sekta ya elimu kuhamasisha utumiaji wa wa chakula bora na salama maskulini
		Kwa kushirikiana na Kamati kiongozi za Afya za Shehia kuielimisha jamii juu ya hatari kuhusu matumizi ya vyakula vyenye kiwango kikubwa cha chumvi, sukari au mafuta
Watu wazima	Lishe ya Mama baada ya Kujifungua.	lunganishwe na maeneo ya programu za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana
	Programu za Uzuiaji wa tumbaku na dawa za kusisimua	Elimisha jamii juu ya hatari ya matumizi ya tumbaku. Kama vile kwa kuvuta au kutafuna.
	Upatikanaji na Utoshelezaji wa Chakula	Elimisha na hamasisha jamii kuhusu uhifadhi wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wake kwa ajili ya familia kwa muda wa mwaka mzima
	Mazoezi ya Viungo	Elimisha na hamasisha tabia ya kufanya mazoezi kwa lengo la kuuweka mwili katika hali ya kiafya kwa maeneo ya kazi na nyumbani.
	Ufanisi wa kuzuia na kushughulikia vihatarishi na maradhi	Kuielemisha jamii juu ya dalili za awali na viashiria vya maradhi yasiyoambukiza. Pendekeza na wezesha utoaji wa huduma za rufaa katika vituo vya afya vilivyo karibu kwa watu wenye dalili za wazi za mardhi ya yasiyoambukiza.

3.2.7 Afua namba 7: Magonjwa Yasiopewa Kipaumbele

Jedwali 14 linatoa muhtasari wa mapendekezo ya huduma za kijamii zitakazotolewa na Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea.

Jedwali 14: Kiwango cha Utoaji wa Huduma kwa ajili ya Maradhi Yasiopewa Kipaumbele

Mikakati	huduma zinatazotolewa
Njia mpya ya udhibiti wa maradhi	Kutoa elimu juu ya Maradhi yasiopewa kipaumbele Kutoa tahadhari juu ya kuongezeka kwa wagonjwa wa maradhi yasiopewa kipaumbele katika maeneo husika na kuyaripoti katika kituo cha afya cha karibu.
Udhibiti wa maradhi yanayosambazwa na mbu	Uambatane na programu za malaria na usafi wa mazingira.
Maji safi na salama, utoaji elimu wahuduma za msingi za usafi wa mazingira na usafi wa mwili	Uambatane na programu za usafi wa mwili, afya na mazingira.

3.2.8 Afua namba 8: Ufuatiliaji na Tathmini

Malengo ya jumla ya vipengele vya tathmini na ufuatiliaji ni kutoa fursa na kufanya tathmini ya ushiriki wa jamii katika mikakati na kuamua ikiwa programu hizi zimeleta mabadiliko yaliyotarajiwa kulingana na vielelezo vya kawaida. Kwa ujumla, Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs) ni muhimu kutoa ripoti ya kila siku kuhusu viashiria vilivyokubaliwa kama vile vifo, ujauzito, mahudhurio ya kliniki za mama wajawazito, ripoti za vihatarishi vya magonjwa kwa kila mwezi na ripoti ya maendeleo ya shughuli ya Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP). Vilevile, CHVs watashiriki katika kufanya tathmini ya wagonjwa, changamoto na kumbukumbu ya utoaji wa huduma, kutoa msaada na kinga zinazotolewa katika kaya kwa ujumla, hasa kwa makundi hatarishi mfano watoto walio katika mazingira hatarishi, watu wenye mahitaji maalumu, watu wenye magonjwa sugu na wazee.

Kuwezesha kurahisisha kufatilia huduma, shughuli pamoja na rikodi zinazotolewa kupitia mikakati iliyojadiliwa hapo juu, wahuduma wa afya wa kujitolea wa jamii wanapaswa kutoa huduma za msingi zifuatazo zinazolingana na ufatiliaji na tathmini katika jedwali la 15.

Jedwali 15: Mkakati wa kijamii kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini

Mkakati	Huduma zinazotolewa na CHV
Data na takwimu	Kutunza kumbukumbu na huduma zote kulingana na makubaliano na maendeleo na viashiria vilivyotengenezwa kwa kila eneo la programu Kufuatilia vifo katika jamii ikiwemo mama na mtoto mchanga ndani ya eneo linalohusika Kushiriki katika shughuli za utafiti kwenye maeneo lengwa
Mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii (CHIS)	Ujazaji wa fomu hasa kupitia katika mtandao zenye taarifa zakuweka na kujumuisha pamoja fomu zote zilizojazwa katika mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii Kuweka kipaumbele katika kuwatembelea miongoni mwa wagonjwa hasa kinamama walio na Umri wa kuzaa na mahitaji yalioelezwa kwenye mpango wa Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Vijana Kutumia njia bora za ufatiliaji wa wagonjwa kuwezesha upatikanaji wa huduma zenye ufanisi rufaa na ukamilishwaji wa rufaa hizo kwa wagonjwa.
Uandishi wa ripoti na usambazaji	Andaa shughuli zote na ripoti za maendeleo kila mwezi na kila robo mwaka kama ilivyoelezwa na msimamizi Kuandaa muhtasari na mrejesho kwa msimamizi wa Kamati za Afya kiongozi katika Shehia, kamati ya ushauriano ya Shehia na jamii kwa ujumla

3.2.9 Programu ya Maswala Mtambuka

Watoa huduma wa afya ya jamii wa kujitolea wanapaswa kushiriki katika programu mtambuka ambazo haziwezi kuonekana kama huduma za moja kwa moja kwa jamii lakini zinaweza kuwa muhimu katika kuwezesha utoaji wa huduma kwa ujumla wake.

Jedwali 16: Kiwango cha utoaji wa huduma kwa ajili shughuli mtambuka

Shughuli	Huduma zinazotolewa na wahudumu wa afya wa jamii wa kujitolea
Uongozi na Utawala	Hudhuria mikutano ya kijamii na utumie kama jukwaa la kutoa elimu ya afya juu ya mada kwa njia tofauti Shiriki katika vikao vya Kamati za Afya Kiongozi katika Shehia (SHCC) yako na utoe mrejesho wa utoaji wa huduma Wakutanishe Masheha, Kamati kiongozi za Afya katika Shehia, kamati ya mashauriano ya Shehia na kituo cha afya katika masuala yanayohusiana na utoaji wa huduma katika jamii
Mipango shirikishi ya Afya	Shiriki katika kuleta maendeleo ya Mpango wa Afya ya Jamii (CBHP) katika Shehia chini ya uongozi wa Kamati Kiongozi za Afya katika Shehia
Uhamasishaji rasilimali	Shiriki katika kufanya kazi na Kamati Kiongozi za Afya katika Shehia katika shughuli za uhamasishaji rasilimali kusaidia utekelezaji wa CBHP katika Shehia
Utayari wa dharura na majibu	Shiriki katika shughuli, utayari wa dharura na majibu kwa kushirikiana na mashirika mengine kama timu za Kikosi Kazi, Ofisi ya Sheha, Kamati Kiongozi za Afya katika Shehia, kamati ya ushauri ya Shehia na vituo vya afya
Magonjwa yanayoibuka	Toa elimu ya afya katika kiwango cha kaya juu ya magonjwa yanayoibuka
Udhalilishaji wa kijinsia	Bainisha na wasilisha matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia

na unyanyasaji wa watoto	
Uhusiano wa Kijinsia	Jumuisha watu wa jinsia zote katika shughuli zote.
Kufundisha na ushauri	Toa elimu ya stadi za maisha kwa wale walio na mahitaji maalumu kwa mtu mmojamoja na kwa vikundi Toa huduma za ushauri juu ya matibabu kwa walemavu na magonjwa maalumu Fikisha huduma na Kutanisha kwa wale walioathiriwa Saidia wote wanaohitaji huduma
Matukio maalumu ya ufuatiliaji	Weka takwimu muhimu za vizazi na vifo Toa taarifa kuhusu maradhi yanayoibuka na wakati wa kukabiliana na dharura Kufuatilia uvumi uliosambaa wa afya katika jamii na kutoa taarifa

Marejeo

1. Admasu K. 2012. The Ethiopian Health Extension Program. Lecture at Johns Hopkins Bloomberg School of Public Health. Baltimore, MD. 8 February 2012
2. Bosch-Capblanch X, Garner P. Primary health care supervision in developing countries. *Trop Med Int Health* 2008; 13(3): 369-83.
3. Creanga AA, Bradley HM, Kidanu A, Melkamu Y, Tsui AO. Does the delivery of integrated family planning and HIV/AIDS services influence community-based workers' client loads in Ethiopia? *Health Policy Plan* 2007; 22(6): 404-14.
4. Crigler L HK, Furth R, Bjerregaard D. . Community Health Worker Assessment and Improvement Matrix (CHW AIM): A Toolkit for Improving Community Health Worker Programs and Services. Bethesda, MD: University Research Co., LLC, 2011.
5. D-Tree. 2020. National CHV Program Service Package. *Presentation*
6. EngenderHealth – Tanzania. 2020. Mafunzo ya Afya ya Uzazi kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea. *Presentation*.
7. Freeman P, Perry HB, Gupta SK, Rassekh B. Accelerating progress in achieving the millennium development goal for children through community-based approaches. *Glob*
8. GHWA Task Force & WHO. Pakistan's Lady Health Worker Programme. World Health Organization & Global Health Workforce Alliance; 2008
9. Godfrey M. Mubyazi, Adiel K. Mushi, Elizabeth Shayo, Kasembe Mdira, Joyce Ikingura, Didas Mutagwaba, Mwele Malecela and Kato J. Njunwa. 2007. Local Primary Health Care Committees and Community-Based Health Workers in Mkuranga District, Tanzania: Does the Public Recognise and Appreciate Them? *Ethno-Med.*, 1(1): 27-35 (2007)
10. Health Extension and Education Center. Health Extension Program in Ethiopia. In: Federal Ministry of Health, editor.; 2007. <http://www.moh.gov.et/english/Resources/Documents/HEW%20profile%20Final%2008%2007.pdf>
11. Henry Perry and Lauren Crigler. 2014. Developing and Strengthening Community Health Worker Programs at Scale. A Reference Guide and Case Studies for Program Managers and Policymakers, Editors: Steve Hodgins, Technical Advisor – USAID. incentives and human resource management tools. *Human resources for health* 2006; 4: 24.
12. Jaskiewicz W, Tulenko K. Increasing community health worker productivity and effectiveness: a review of the influence of the work environment. *Human resources for health* 2012; 10(1): 38.
13. Laughlin M. The Care Group Difference: A Guide to Mobilizing Community-Based Volunteer Health Educators. Baltimore, MD: World Relief and the Child Survival Collaborations and Resources (CORE) Group; 2004.
14. Lauren Crigler, Jessica Gergen, and Henry Perry. 2013. Supervision of Community Health Workers. K4Health. (www.k4health.org/.../Directly-observed%20Supervision%20Checklists. Management (iCCM): Stakeholder Perceptions and Priorities. *Am J Trop Med Hyg* 2012;
15. Massenga, J.; Noronha, R.; Awadhi, B.; Bishanga, D.; Safari, O.; Njonge, L.; Kim, Y.-M.; Roosmalen, J.v.; van den Akker, T. 2021. Family Planning Uptake in Kagera and Mara Regions in Tanzania: A Cross-Sectional Community Survey. *Int. J. Environ. Res. Public Health* 2021, 18, 1651. <https://www.mdpi.com/1660-4601/18/4/1651>
16. Mathauer I, Imhoff I. Health worker motivation in Africa: the role of non-financial
17. MOH. 2007. Community Based Roll Back Malaria Initiative. Experience From Jambiani (1997 – 2007).
18. MOH. 2011. Behaviour Change Communication Toolkit for Shehia Health Custodian Committees. The Revolutionary Government of Zanzibar
19. MOH. 2013. Mwongozo wa Mwezesaji kwa Wawezeshaji wa Kamati Kiongozi za Afya za Shehia. Seikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
20. MOH. 2014. Mwongozo wa Kukusanya Taarifa za Afya Kutoka Katika Jamii (Shehia) Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
21. MOH. 2015. National Guidelines for Integrated Community Based Health Care. The Revolutionary Government of Zanzibar
22. MOH. 2017. Assessing Knowledge, Attitude, Practice and Behaviour Related to Malaria Among The General Population in Zanzibar. Ministry of Health Zanzibar.

23. MOH. 2018. Planning and Implementation of District Health Services.
24. MOH. 2018. Zanzibar Malaria Elimination Social and Behavior Change Communication (SBCC) Strategy (2018-2023). The Revolutionary Government of Zanzibar.
25. MOHCDGEC. 2019. Manual for Management of Tuberculosis and Leprosy in Tanzania. The United Republic of Tanzania.
26. MOHSW. 2009. Zanzibar Health Policy. The Revolutionary Government of Zanzibar.
27. MOHSW. 2012. Health Information System Strategic Plan (2012-2020). The Revolutionary Government of Zanzibar
28. MOHSW. 2013. Zanzibar Health Sector Strategic Plan III (2013/14-2018/19). The Revolutionary Government of Zanzibar
29. MOHSW. 2017. National Guidelines on Comprehensive HIV Interventions for Key Populations (KPs) In Zanzibar. The Revolutionary Government of Zanzibar
30. MOHSWEGC. 2019. Zanzibar Community Health Strategy (2019–2025). The Revolutionary Government of Zanzibar
31. MOHSWEGC. 2020. Mpango wa Taifa wa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea: Mwongozo wa Mafunzo ya Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea. Seikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
32. MOHSWEGC. 2020. Mpango wa Taifa wa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea: Mwongozo wa wa Mwalimu wa Kufundishia Wahudumu wa Afya ya Jamii wa Kujitolea. Seikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
33. MOHSWEGC. 2020. Zanzibar Digital Health Strategy 2020/21 - 2024/25. The Revolutionary Government of Zanzibar
34. MOHSWEGC. 2020. Zanzibar National Guidelines for the Prevention and Treatment of HIV AND AIDS. The Revolutionary Government of Zanzibar
35. Moses Mulumba, Leslie London, Juliana Nantaba, and Charles Ngwenya. 2018. Using Health Committees to Promote Community Participation as a Social Determinant of the Right to Health: Lessons from Uganda and South Africa. *Health and Human Rights Journal*. Volume 20: Number 2.
36. Oxford Policy Management. Lady Health Worker Programme: Fourth External Evaluation for the National Programme for Family Planning and Primary Health Care- Quantitative Survey Report, 2009. <http://www.opml.co.uk/projects/lady-health-worker-programme-thirdparty - evaluation-performance>
Public Health 2009; 1-20. Retention of Community Health Workers Delivering Integrated Community Case
37. Selemani Mbuyita, Hadija Kweka, Ahmad Makemba na D. Mboya. 2010. Mwongozo wa Kufundishia. Mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati za Afya za Vituo vya Tiba. Ifakara Health Institute.
38. Stekelenburg J, Kyanamina SS, Wolffers I. Poor performance of community health workers in Kalabo District, Zambia. *Health Policy* 2003; 65(2): 109-18.
39. Strachan DL, Kallander K, Ten Asbroek AH, et al. Interventions to Improve Motivation and
40. Teklehaimanot A, Kitaw Y, Yohannes AM, et al. Study of the Working Conditions of Health Extension Workers in Ethiopia. *Ethiopian Journal of Health Development* 2007; 21(3): 246- 59
41. Willows International – Tanzania. 2020. Formalization and Revitalization of the Shehia Health Custodian Committees (SHCCs) in Urban West Region, Zanzibar. Regional Administration and LG Meeting. *Presentation*.
42. Willows International – Tanzania. 2020. Interpersonal Communication. A Program to Help Women Meet Their Reproductive Health Needs. *Presentation*.
43. Willows International – Tanzania. 2020. The Zanzibar Program. *Presentation*.
44. Willows International – Tanzania. 2021. SHCC formalization status Report by 29th January 2021, West Urban Region. *Report*.
45. Willows International. 2018. A Program to Help Women Meet Their Reproductive Health Needs: Field Educator Training - Trainer's Manual.

Kiambatisho 1

Hadidu Rejea Kwa Timu ya Wataalamu wa Afya ya Jamii

Utangulizi

Mfumo wa sasa wa utoaji wa huduma za afya Zanzibar ulijumuishwa katika utendaji wa idara kuu na programu zinazosimamia maradhi. Ugawaji wa malighafi na vitendea kazi kwa utoaji wa huduma umekuwa ukiegemea zaidi katika baadhi programu hizo., na ambapo kila moja ya programu ina mfumo wake wa utoaji wa huduma, hali ambayo imesababisha kuelemea katika ugawaji wa huduma kulingana na matakwa ya wanaotoa huduma hizo.

Kutokana na hii, kumekuwa na mfumo usiofaa na usio na usawa pamoja na mkanganyiko wa mikakati ambao ulisababisha mfumo wa ugawaji wa malighafi na vitendea kazi na kusababisha ushiriki dhaifu katika kupanga mkakati wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora za afya katika ngazi ya wilaya, hii ni kutokana na kwamba mpango huu uliratibiwa na kutekelezwa kutoka ngazi za juu. Jambo ambalo lilisababisha muingiliano na mtawanyiko wa wafanyakazi wa wilaya katika ngazi za juu wakati wa utekelezaji wa mpango wa afya wa Wilaya.

Kutokana na changamoto hiyo ya utoaji wa huduma, hali hii imesababisha mrundikano wa shughuli nyingi kuliko zilivyohitajika baina ya jamii na watoa huduma za afya kwa namna fulani au kutoshiriki na kutoshirikishwa kwa jamii katika hatua zote za ubainishaji, upangaji na ufuatiliaji wa tathmini.

Kutokana na hali hii iliyosababisha mazingira mabaya utekelezaji wizara kufahamu vipaumbele vyake vya utekelezaji wa mikakati ya uwekezaji fedha katika afya. Wizara iliona ni vigumu kutekelezwa kwa ufanisi mpango huo, na kushirikishwa kwa jamii kikamilifu na kuhakikisha kuwa mikakati hiyo ya mpango wa afya ingedumu na kuwa endelevu katika jamii na kuweza kukubaliwa. Kwa hivyo, mpango wa afya ya jamii Zanzibar ulianzishwa ili kuhakikisha mambo yafuatayo; -

- Kuongezwa nguvu za ziada zinazohitajika katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya kulingana na hali ya sasa ili kuhakikisha huduma zinazotolewa ni sahihi na zenye ufanisi
- Kuwepo kwa mahitaji ya huduma bora inayotokana na mahitaji ya walengwa
- Wateja/jamii wamewezeshwa kufanya maamuzi juu ya vipaumbele na mgawanyo wa rasilimali
- Kutilia mkazo mipango na utekelezaji yenye ufanisi katika ngazi za wilaya kuwa ni kama sekta kuu ya utoaji wa huduma utakaoweza kutumika katika mazingira na hali tofauti ili kukabiliana na mahitaji ya kijamii ambayo yatakuwa na ufanisi na jumuishi (ushajiishaji, kinga, tiba na njia za kuhudumia wagonjwa vizuri
- Kwa ufanisi kuingiza miundo iliyopo inayohusika na upangaji wa afya katika ngazi ya jamii na Kamati kiongozi za Afya katika Shehia ili kutimiza na kusaidia kukamilisha kazi muhimu zinazoambata na na utoaji wa huduma.

Kwa ujumla, hadidu rejea hizi, (TOR) za Afya ya Jamii kimsingi zitahitaji kutilia mkazo kutekelezwa matakwa ya Serikali ya kuweka mpango bora wa Afya ya Jamii wenye viwango vya usawa, vilivyo sanifishwa na vilivyounganishwa kwa Afya ya Jamii kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea (CHVs)), Kamati kiongozi ya Afya ya Shehia (SHCCs) na Mfumo wa Habari ya Afya ya Jamii (CHIS) uliyounganishwa na Mfumo wa Taarifa wa Afya ya Wilaya (DHIS-2). Mkazo huu muhimu sana wa kimkakati unasisitizwa vivyo hivyo katika Mkakati wa Afya ya Jamii ya Zanzibar,(ZCHS 2019-2025) ambayo inaambatana na maeneo maalum ya kimazingira kama vile kuwekwa kwa taasisi ya utoaji wa huduma ya afya ya jamii; Watoa huduma wa Afya wa kujitolea wa jamii (rasilimali watu); mifumo ya jamii na miundo ya umiliki na uwajibikaji kama Kamati za za mashauriano za Shehia, Kamati kiongozi ya Afya ya Shehia (SHCCs) na bodi za habari, mawasiliano na teknolojia; uongozi, uwajibikaji na uratibu katika ngazi zote.

Hadidu Rejea za Timu ya Wataalamu wa Afya ya Jamii

- Kutoa msaada wa kitaalamu kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia, na Watoto, kwa kuandaa miongozo ya kawaida ya kamati Kiongozi za Afya za Shehia ndani ya mfumo wa sheria wa Zanzibar na ugatuuji wa huduma chini ya Serikali za Mitaa.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri katika kutekeleza Mpango wa Afya ya Jamii Zanzibar wa mwaka 2019-2025 kwa vitendo ili kuimarisha utendaji kazi wa Kamati za Afya za Shehia, Kamati

Kiongozi katika Shehia Zanzibar pamoja na usanifishaji, ujumuishaji na uratibu wa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea.

- Kutoa msaada wa kitaalamu kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ili kufikia utekelezaji ulioratibiwa vizuri kwa kuimarisha Mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii ili kuwa na uhusiano mzuri kati ya jamii na mifumo ya msingi ya utoaji wa huduma za afya.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri katika maendeleo ya kina na uratibu mzuri ili kukidhi viwango vya utoaji wa huduma, miongozo na mchakato wa usimamizi baina ya Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea na Kamati Kiongozi za Afya za Shehia kulingana na muktadha wa mahitaji yaliyowekwa kama inavyoonekana katika Mpango wa Afya wa Zanzibar.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri kwa kuweka pamoja, uwekaji wa viwango sawa na ujumuishaji wa Mpango wa Afya ya Jamii ili kufafanua Kiwango cha utoaji wa huduma za afya kutoka katika Afua lengwa za afya ikiwa ni pamoja na Afya ya uzazi, Mama, Mtoto na Vijana, Kifua Kikuu na VVU / UKIMWI, Malaria pamoja na ufuatiliaji wamaradhi ya kikanda yaliyopuuzwa, maradhi yasiyoambukiza, afya ya mwili na usafi wa Mazingira na Makuzi ya awali ya Mtoto.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri kwa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuweka mbinu ya kitaifa ya uanzishaji mafunzo na msaada kwa kuhakikisha usambazaji wa kutosha na wa haki kwa Wahudumu wa Afya wa Jamii wa Kujitolea na Kamati Kiongozi za Afya katika Shehia.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri wa kuaminika na unaofaa katika upatikanaji wa takwimu za Mfumo wa taarifa za Afya ya Jamii katika mfumo wa taarifa wa Afya wa Wilaya ili kutoa ushauri bora, mipango, upangaji na uwekaji wa vipaumbele katika ngazi ya jamii na kituo cha afya.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri juu ya programu ya mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Uangalizi wa Afya ya Shehia ikiwa ni pamoja na kuwapatia ujuzi wa kupanga kipaumbele, upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji katika muktadha wa mipango ya wilaya.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri kwa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto juu ya muundo na utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa wa Jamii na kusimamia mfumo huo kutoka na miongozo inayofanana ambayo ni rahisi kufikiwa na kutumiwa katika ngazi ya jamii.
- Kuisaidia na kuishauri Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia, na Watoto juu kufuatilia maboresho katika utendaji wa Kamati za Afya za Shehia.
- Kufanya utafiti na shughuli zinazohusiana na Afya ya Jamii Zanzibar ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na kutumia matokeo kwa maendeleo ya jamii.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri juu ya uanzishwaji na usimamizi wa Timu ya Wakufunzi ya Kitaifa Zanzibar.
- Kutoa msaada wa kitaalamu na ushauri juu ya utaratibu mzuri wa kuratibu mbinu na kuboresha Mpango wa Afya ya Jamii Zanzibar.